**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NANE

## KIKAO CHA SABA

**13 SEPTEMBA, 2017**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA NANE

## KIKAO CHA SABA – TAREHE 13 SEPTEMBA, 2017

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Maelezo ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Reli wa Mwaka 2017 *(The Railways Bill, 2017).*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Reli wa Mwaka 2017 *(The Railways Bill, 2017).*

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Maoni ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu

Muswada wa Sheria ya Reli wa Mwaka 2017 *(The Railways Bill, 2017).*

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**82. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali ilikuwa na mpango wa kuanzisha Kata mpya ya Mkanana ambayo ina Vijiji vya Mkanana na Chibwegele na vipo mlimani ambapo hakuna huduma yoyote kama vile barabara ambayo ni mbaya sana na hupitika kwa shida wakati wote:-

(a) Je, mpango huo wa kuanzisha Kata mpya umefikia wapi;

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kuanzishwa kwa Kata hiyo kutawezesha kuwasogezea karibu huduma mbalimbali Wananchi wa Kata hiyo kuliko ilivyo sasa ambapo Makao Makuu yapo Kijiji cha Chitemo umbali wa km 45.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

**83. MHESHIMIWA MOHAMED OMARY MCHENGERWA (RUFIJI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Ni takribani miaka miwili sasa Serikali imeshindwa kuwahakikishia Wananchi wa Jimbo la Rufiji kuwa na umeme wa uhakika kufuatia hitilafu ya mara kwa mara kwenye mitambo ya umeme unaozalishwa na gesi kutoka Kilwa:-

Je, ni lini Serikali itawaunganisha Wananchi wa Rufiji, Kibiti na Kilwa kwenye Grid ya Taifa.

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

**84. MHESHIMIWA KHADIJA NASSIR ALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

(a) Je, ni vifaa gani muhimu vimewekwa kwenye vifungasho vya akina Mama wakati wa kujifungua *(delivery kit)* takribani laki tano (500,000) zinazokusudiwa kusambazwa na Serikali;

(b) Je, ni kwa nini Serikali inasuasua kwenye usambazaji wa “*delivery kit”* kama mkakati ulivyo;

(c) Je, ni kwa kiasi gani agizo la Mheshimiwa Mwandosya la Serikali la kuanzisha huduma za upasuaji kwenye Vituo vyote vya Afya nchini limetekelezwa.

**85. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:- Kwa kuzingatia umuhimu wa taulo za kike nchini:-

Je, Serikali inaonaje ikiondoa kodi kwenye taulo hizo.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**86. MHESHIMIWA ELIAS JOHN KWANDIKWA (USHETU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuboresha maeneo ya uendeshaji na usimamizi wa rasilimali ya Menejimenti, Bodi, Mabaraza ya Madiwani, Ukaguzi wa nje, Ukaguzi wa ndani na

kuliacha eneo muhimu la Kamati za Ukaguzi *(Audit Committee)* kwenye Wizara, Idara, Wakala na Serikali za Mitaa:-

Je, ni lini Serikali itaboresha Kanuni ili Muundo wa Kamati za Ukaguzi ziundwe na Wajumbe wengi *(majority)* toka nje ya Taasisi kwa kuzingatia weledi na uzoefu ili kusimamia rasilimali kwa tija na ufanisi.

**87. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Serikali ilitangaza kuzinyang'anya Halmashauri uwezo wa kukusanya mapato ya Kodi ya Majengo *(property tax)* na kuagiza kodi hiyo kukusanywa na Mamlaka ya Mapato (TRA):-

(a) Je, baada ya Mamlaka ya Mapato kupewa jukumu hilo, ufanisi umefikiwa kwa kiasi gani ikilinganishwa na mapato yaliyokuwa yakikusanywa na Halmashauri zenyewe;

(b) Kwa kuwa Kodi ya Majengo ilikuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa mapato ya Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji na majukumu ya kutoa huduma kwa Wananchi

hayajapunguzwa; Je, Serikali imejipanga vipi kufidia vyanzo hivyo vilivyopotea.

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

**88. MHESHIMIWA DANIEL EDWARD MTUKA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kwa kuwa Bwawa linalotarajiwa kuchimbwa katika Kijiji cha Mbwasa, Tarafa ya Kintinku ni Bwawa la kimkakati kwa Wakazi wa Tarafa nzima ya Kintinku:-

Je, ni lini Serikali itaanza rasmi ujenzi wa Bwawa hilo baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika.

**89. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Serikali imekamilisha mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Mji wa Ngudu na Vijiji vilivyo karibu na Mji huo Wilayani Kwimba. Mradi huo unatoa maji ya uhakika kuliko miradi ya visima vifupi ambavyo ni vya msimu. Lakini Mji Mdogo wa Malampaka na Vijiji vingine vya karibu kama Jihu, Bukigi, Muhida, Lali, Nyabubinza na

Mwang'honoli ambavyo vipo karibu na Mji wa Ngudu havijaunganishwa kwenye mradi huo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunganisha Mji Mdogo wa Malampaka na Vijiji vya Jihu, Bukigi, Muhida, Lali, Nyabubinza na Mwang'honoli katika mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria ili kuwapatia Wananchi maji ya uhakika.

**90. MHESHIMIWA MAGDALENA HAMIS SAKAYA (KALIUA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Wilaya ya Kaliua inakabiliwa na tatizo kubwa sana la maji hali inayosababisha Wananchi wake wengi kuteseka kwa kukosa huduma hiyo muhimu na kutumia muda mwingi kutafuta maji umbali mrefu na hivyo kushindwa kufanya shughuli za maendeleo:-

Je, mradi mkubwa wa kutoa maji katika Mto Malagarasi kwenda Vijiji vya Kaliua mpaka Urambo utaanza lini na kukamilika lini.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

### 91. MHESHIMIWA GOODLUCK ASAPH MLINGA (ULANGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Rais wa Awamu ya Tano aliahidi kuwapatia Wananchi wa Kata za Lupiro Iragua, Milola na Miwepa eneo la ardhi oevu ya Bonde la Mto Kilombero kwa ajili ya Makazi na Kilimo pindi tu atakapoingia madarakani:-

Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia wapi.

### 92. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (SAME MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Je, ni lini Serikali itatengeneza miundombinu ya maji katika Hifadhi ya Mkomazi ili kuzuia Wanyamapori kuzurura kwenye makazi ya Wananchi wakitafuta maji na kuharibu mazao yao.

## WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

### 93. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Je, ni lini Serikali itawapatia Wananchi wa Kyerwa haki yao ya kusikiliza Radio ya Taifa (TBC Taifa) ili kujua yanayoendelea katika nchi yao kama ilivyokuwa hapo awali kabla ya kubadilisha teknolojia ya habari na badala yake sasa wanasikiliza Radio za Rwanda na Uganda.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

### 94. MHESHIMIWA ENG. ATASHASTA JUSTUS NDITIYE (MUHAMBWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Gereza la Wilaya ya Kibondo – Nyamisati limekuwa na ongezeko kubwa sana la Wafungwa na Mahabusu kwa sababu ya uwepo wa Wakimbizi:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati unaofaa kupeleka mradi mkubwa wa maji kwenye Gereza hilo ili kulinda afya za raia na Askari walioko kwenye Gereza hilo.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**95. MHESHIMIWA GIMBI DOTTO MASABA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) katika Mkoa wa Simiyu na kukijengea uwezo wa kutengeneza vifaa kama vile baiskeli, pikipiki na magari.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu).***

Muswada wa Sheria ya Reli wa Mwaka 2017 *(The Railways Bill, 2017).*

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**13 SEPTEMBA, 2017** **KATIBU WA BUNGE**